

Ramadhan Njia ya Mafanikio

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Kitabu Chake kitukufu:

«شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنْزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ».

“Mwezi wa Ramadhan ambao imetéremshwa humo Qur’ani kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi”. Mwezi mtukufu wa Ramadhan ni wakati muafaka kwetu sisi Waislamu kuzingatia na kutafakari upya jinsi tulivyo karibu na Mola Mlezi wetu (swt), na vilevile jinsi tunavyoliona lengo na kipimo chetu cha kweli maishani, na jinsi tunavyofafanua maana ya mafanikio katika maisha na jinsi tunavyoyafikia. Ni mwezi ambao unashikilia ndani yake uwezo wa kutupa “njia ya mafanikio.”

Katika jamii tunazoishi ndani yake, tumezungukwa na mitazamo mingi, athari, na mashinikizo yanazoweza kutengeneza mtazamo wetu wa mafanikio. Lakini upi ufanuzi wa Muumba kuhusu mafanikio? Je, tutayafikiaje kupitia matendo yetu binafsi, ndoa zetu, maisha ya familia zetu, mambo yetu ya kifedha, na vipengee vyengine vya maisha yetu? Je, ni upi mtazamo sahihi wa mwanamke aliyefanikiwa kwa mujibu wa Uislamu? Zaidi ya hayo, Muislamu anatafuta mafanikio si kwa ajili yake tu, bali hata kwa Umma wake wa

Kiislamu na dini yetu ya Kiislamu. Je, sisi kama Umma wa Kiislamu tunapaswa kuutazama vipi Umma na dola iliyofanikiwa na iliyoendelea, na tunawezaje kufikia lengo hili? Je, ni kichocheo gani cha mafanikio cha kutatua matatizo mengi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii tunayokabiliana nayo kwa sasa, na ni zippi sifa za harakati au chama chenye mafanikio ili kufikia mabadiliko ya kweli katika nchi zetu na kwa wanadamu?

Tutashughulikia maswali haya na mengine katika maudhui yetu ya mwezi huu uliobarikiwa katika Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir: “Ramadhan: Njia ya Mafanikio.” Mnaweza kufuatilia warsha ya Ramadhan kwenye link iliyopo hapo chini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu maudhui hizi ziwe ni njia ya kuangaza njia kwa Umma huu kufikia mafanikio ya kweli hapa duniani na kesho akhera, Mungu Mungu akipenda.

«ذَكَرُ الْكِتَابِ لَا رَيْبٌ فِيهِ هُدًى لِلْمُتَّقِينَ * الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ وَيَقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمَا رَأَيْنَاهُمْ يَنْفَعُونَ * وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنْزَلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنْزَلَ مِنْ قَبْلِكَ وَبِالآخِرَةِ هُمْ يُوْقَنُونَ * أُولَئِكَ عَلَىٰ هُدًىٰ مِنْ رَبِّهِمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلُحُونَ»

“Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni uwongofu kwá wachamungu.”

Ambao huyaamini ya ghaibu na hushika Sala, na hutoa katika tuliyo wapa. Na ambao wanayaamini yaliyo teremshwa kwako, na yaliyo teremshwa kabla yako; na Akhera wana yakini nayo. Hao wapo juu ya uwongofu utokao kwa Mola wao Mlezi, na hao ndio walio fanikiwa.” [Al-Baqara: 2-5]



#Gateway2Success



HT-CMO-WS



WSCMOHT1924



WOMENSHARIAH5